**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA URAMBO**
**S.L.P 211, URAMBO,TABORA.**
SIMU NA. 0620676734/0786930095(MKUU WA SHULE) 0714347234 /0764485623(MAKAMU)

**SHULE YA SEKONDARI URAMBO**

**Unapojibu tafadhali taja:**
**KUMB.NA.URB//SEK/SEL/11.**
**Kwa mzazi/mlezi wa.................................**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI URAMBO KIDATO CHA TANO MWAKA 2024/2025**

Napenda kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika shule ya sekondariUrambo Shule inakupongeza kwa kupata nafasi hii.

Shuleya sekondari Urambo ipo Mkoa wa Tabora,Wilaya ya Urambo, tarafa ya Urambo. Ni umbali wa kilometa (3) kutoka mjini Urambo kuelekea barabara ya Ulyankulu, kaskazini mwa mji wa Urambo.

Muhula wa kuanza masomo unaanza tarehe ..................... Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe .................. na mwisho wa kuripoti ni tarehe ............

Unatakiwa kuripoti shuleni tarehe iliyotajwa hapo juu ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule utapokelewa na kuingizwa kwenye rejesta ya shule utakapokuwa UMETIMIZA mambo yaliyomo kwenye viambatanisho A mpaka D na kukabidhi au **kuwasilisha kivuli (nakala picha) ya cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa pamoja na matokeo ya kidato cha nne au Result Slip.**

A. MAAGIZO MAALUM

B. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

C. FOMU YA KUJIUNGA NA SHULE

D. FOMU YA KUPIMWA HOSPITALI

**KIAMBATANISHO 'A'**

**MAAGIZO MAALUM.**

**1. SARE ZA SHULE**

(i) (a) Sketi ndefu za kitambaa kizito za darasani mbili (02) DARK GREEN (ya malinda) zifike kwenye kiwiko cha mguu.

(b) Sketi za kushindia mbili (02) DAMU YA MZEE zenye marinda ya kawaida ndefu zinazofika kwenye kiwiko cha miguu.(ankle)

(ii) Shati mbili (02) nyeupe tetron za mikono mirefu, zisibane mwili wako.

(iii) T-shirt mbili (02) za rangi ya kijivu mpauko nzito zisizo na kora na ambazo hazina maandishi yoyote.

(iv) Viatu vyeusi vya ngozi vya ngozi vinavyofunika miguu vyenye kamba visivyo na kisigino (usinunue simple shoes).

(v) Sweta DARK GREEN, moja (01).

(vi) Soksi (stocking) nyeupe ndefu jozi mbili au zaidi.

(vii) Nguo za michezo (raba nyeupe na track suit rangi ya bluu).

**NB:** ***Wakati wa kuja shuleni njoo ukiwa umevaa sare za shule kwani nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa.***

**2. MICHANGO YA SHULE.**

- Michango ya uendeshaji wa shule - Tshs 65,000/=
- Tahadhari - Tshs 5,000/=
- Kitambulisho - Tshs 5,000/=
- Nembo - Tshs 5,000/=

**JUMLA YA MICHANGO YOTE NI TSHS 80,000/= FEDHA HIZI LIPIA NMB AKAUNTI NAMBA:51301100062. JINA LA AKAUNTI: URAMBO SECONDARY SCHOOL CAPITATION** (kwenye Bank Pay in Slip ni muhimukuandika jina la mwanafunzi na kidato/ darasa analoanza kusoma).

**NB: Njoo na Bank Pay in Slip za malipo yote, fedha taslimu hazitapokelewa.**

**3. MAHITAJI YA BWENINI.**

(i) Sanduku la chuma

(ii) Taa ya dharula (solar)

(iii) Chandarua chenye dawa cha rangi ya bluu kisicho na urembo.
(iv) Mswaki na dawa ya meno ya kutosha muhula
(v) Sabuni za kufulia na kuogea.
(vi) Vifaa vya kulia chakula (sahani, bakuri, kikombe na kijiko) visiwe vya plasitiki.
(vii) Ndoo mbili (02) ndogo za plastiki kwa ajili ya kuogea na kufulia.
(viii) Mto mmoja na foronya mbili (02) za rangi ya bluu.
(ix) Shuka mbili au zaidi za rangi ya bluu na Blanketi moja (01).
(x) Fedha za matumizi madogomadogo pamoja na nauli ya kurudi nyumbani shule itakapofungwa.
(xi) Gharama za godoro ni tsh. 20,000/= kwa miaka miwili kwa wanafunzi 134 watakaowahi kuripoti na inalipwa kwa pamoja shuleni siku ya kuripoti. Aidha watakaochelewa watalazimika kununua godoro kwani shule ina idadi ndogo ya godoro.

**4. MAAGIZO MENGINE.**
(i) Madaftari (Counter book 3Q yanayotosha masomo yako yasipungue 12.
(ii) Vitabu vya ziada kwa masomo yako angalau kitabu kimoja kwa kila somo.
(iii) Njoo na "Disection tray (kwa wanaosoma CBG) kubwa na zenye nta ya kutosha
(iv) Kalamu za wino za kutosha muhula mzima.
(v) Rimu mbili (02) za karatasiaina ya A4).
(vi) Scientific calculator (fx -991ms CASIO) na Mathematical set kwa wanafunzi wa CBG.
(vii) Njoo na kamusi ya kiingereza kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya sanaa (Arts)
(viii) File la kuwekea kumbukumbu ya mitihani ya ndani na rimu moja ya karatasi ($A_4$).
(viii) Vifaa vya usafi.

- Jembe lenye mpini mrefu
- Ufagio wa ndani (soft bloom mmoja (01).
- Ufagio mgumu wa kusugua sakafu (hard bloom).
- Ufagio laini wa kudekia sakafu (squizer)
- Kwanja (slesher ) moja (01) kwa usafi wa mazingira

**ANGALIZO:**
1. Hauruhusiwi kuja na nguo za nyumbani.
2. Hauruhusiwi kuja na manukato (perfume, wanja, lipbam, rangi za kucha n.k.
3. Kwa wanafunzi wanaovaa hijabu washone sketi ndefu, shati la mikono mirefu, Na juba mbili (02) za darasani na mbili za kijivu kwa ajili ya kushindia/kazi za nje.
4. Hauruhusiwi kuja na pasi ya umeme.
5. **Hauruhusiwi kuja na vifaa vifuatavyo, simu za mkononi, radio, camera n.k atakayebainika na vifaa hivi atafukuzwa shule.**
6. Vyakula vya aina yoyote mf. Mkate, pipi, biskuti, sukari n.k haviruhusiwi kuja navyo.
7. Hairuhusiwi kusuka nywele
8. Sketi zote zitakazoshonwa (za darasani na kushindia) ziwe ndefu za kufunika kiwiko cha mguu.

**MUHIMU KWA MZAZI NA MWANAFUNZI**

1. Kwa mawasiliano na mwanao anapokuwa shuleni TUMIA NAMBA HIZI:-
   . 0620676734/0786930095 (MKUU WA SHULE) au 0714347234/0764485623 (MAKAMU MKUU WASHULE) na si vinginevyo.
2. Ni marufuku kwa mwanafunzi na mzazi/mlezi kutumia mawasiliano tofauti na namba zilizoelekezwa hapo juu ikibainika kuwa mwanafunzi anatumia simu tofauti na hizo namba zilizoelekezwa kuwasiliana na mzazi/mlezi au mtu yeyote atafukuzwa shule.
3. Ni muhimu kumpatia mwanao fedha za kutosha kujikimu au fedha za matumizi binafsi kama matibabu na dharura nyinginezo awapo shuleni. Kumbuka hudhurio moja tu la kumwona daktari pale anapokuwa mgonjwa siyo chini ya Tshs 5,000/= bila dawa.
4. Siku za kuripoti shuleni ni kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa kabla ya saa kumi kamili jioni (yaani siku za kazi na muda wa kazi tu).
   Mwanafunzi akifika shuleni aripoti ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule kwa ajili ya ukaguzi na usajili kabla hajaenda bwenini. Ni kosa kuingia bwenini kabla ya kukaguliwa na Ofisi ya Makamu Mkuu wa Shule na kupokelewa.
6. Mzazi/mlezi unaruhusiwa kuja kumtembelea mwanao kila JUMAMOSI ya mwisho wa mwezi kwa lengo la kujua maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma na kinidhamu.Tafadhali usije na vyakula vya aina yoyote kama vile chipsi, maji, biskuti, juice n.k

**KIAMBATANISHO 'B'**
**SHERIA ZA SHULE.**
**A. SHERIA ZA JUMLA**

**1:0. HESHIMA.**

1:1. Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa wimbo waTaifa na fedha za Taifa.
1:2. Mwanafunzi anatakiwa awe MFANO mzuri wa HESHIMA NA TABIA popote atakapokuwa.
1:3. Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu WAFANYAKAZI WOTE WA SHULE, kujiheshimu yeye mwenyewe na kuwaheshimu wanafunzi wenzake.
1:4. Mwanafunzi anapaswa kusimama na kuwasalimu wakubwa mahali popote anapokutana nao.
1:5. Mwanafunzi AJIHADHARI NA KAULI CHAFU kwa jamii nzima.

**2:0. MAHUDHURIO.**

2:1. Mwanafunzi anapaswa kufika shuleni saa 1:10 asubuhi na kuhudhuria paredi saa 1:30 kila siku za masomo.
2:2. Mwanafunzi anapaswa kufika shuleni saa 1:10 asubuhi na kuhudhuria vipindi vyote bila kutokatoka nje ya darasa wakati wa masomo pia ni marufuku kupiga kelele au kufanya usumbufu wa aina yoyote darasani.
2:3. Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria na kushiriki kikamilifu katika kazi za mikono kulingana na maagizo/ratiba ya shule.
2:4. Mwanafunzi anapaswa kutii kengele ya shule kulingana na utaratibu au ratiba ya shule.
2:5. Mwanafunzi HARUHUSIWI KUTOKA nje ya eneo la shule bila KIBALI CHA MAANDISHI kutoka kwa mwalimu wa zamu au darasa.

2:6. Mawasiliano yote kutoka kwa wazazi /walezi yanayomuhusu mwanafunzi kama vile msiba/magonjwa n.k yatafanywa na ofisi ya mkuu wa shule.

**3:0. NIDHAMU.**

3:1. Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya shule ya Urambo sekondari wakati wote akiwa shuleni au sehemu nyingine kama itakavyoelekezwa na viongozi wa shule. Shati ni lazima lichomekewe na viatu vivaliwe pamoja na soksi.

3:2. Kila mwanafunzi kwa vyovyote vile ni lazima kuhudhuria vipindi vya dini kulingana na dini yake.

3:3. Kila mwanafunzi anapaswa kutii wito wa kengele kulingana na utaratibu wa shule.

3:4. Ruhusa ya kulala nje ya shule kwa sababu maalumu itatolewa na Mkuu wa shule au Makamu wake tu.

3:5. Kila mwanafunzi lazima aheshimu kazi za mikono zitakazotolewa kulingana na utaratibu.

3:6. Mwanafunzi anapaswa kujali na kutunza mali za shule mf. Taa za umeme, miundombinu ya maji, kuepuka kuchora kwenye kuta, kwani uharibifu wowote utakaojitokeza kwa uzembe wa mwanafunzi utagharimiwa na mwanafunzi mwenyewe.

3:7. Sare za shule ni lazima zivaliwe wakati wa masomo na wakati wa kuruhusiwa kutoka nje ya shule.

**TANBIHI:** Nywele zitunzwe na ziwe fupi, Na ni marufuku kunyoa vipara au panki, kuvaa nguo za kubana na kuonyesha maumbo ya mwil, kufuga kucha ndefu, mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele hata kama anavaa hijabu.

**4:0. MAENEO YASIYORUHUSIWA:**

4:1. Mwanafunzi asitembelee maeneo yafuatayo ila tu kwa ruhusa maalumu maeneo hayo ni:-
- Ofisi za shule na idara zake kama vile sehemu ya kuchapia na kurudufishia mitihani.
- Bohari ya shule.
- Maabara
- Nyumba za walimu/wafanyakazi.

4:2. Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea vilabu vya pombe, na nyumba za kulala wageni.

**5:0. WAGENI:**

Mwanafunzi haruhusiwi kutembelewa na mgeni yeyote tofauti na mzazi/mlezi. Mzazi/mlezi ana ruhusiwa kumtembelea mwanafunzi siku ya Jumamosi ya kila mwisho wa mwezi tu. **Mgeni huyo awe Mzazi au Mlezi, anayetambuliwa na uongozi wa shule, na ambaye picha zake za paspoti zimeambatanishwa katika fomu hii na aonane na mwanafunzi kwa ruhusa ya mwalimu wa zamu, mwalimu wa malezi au mwalimu wa bweni.** Hata hivyo shule haina nafasi ya kulaza mgeni /wageni wa mwanafunzi.

**B. SHERIA ZA DARASANI.**

1. Darasani ni mahali pa kujifunzia, kelele za aina yoyote haziruhusiwi kila mwanafunzi anatakiwa kukaa kwa taratibu zilizowekwa na mwalimu wa darasa.
2. Mahudhurio darasani ni lazima kwa kila mwanafunzi wakati wa vipindi na muda mwingine wakujisomea ambao umepangwa na shule. Mwanafunzi mtoro atafukuzwa shule.
3. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa kwenye meza au kiti cha mwalimu.
4. Kila mwanafunzi ni lazima afanye usafi wa darasa kulingana na ratiba iliyopo.

5. Hairuhusiwi kufanya kikao chochote darasani bila ruhusa ya mwalimu wa darasa au mamlaka nyingine.

**C. SHERIA ZA BWENINI.**

1. Bwenini ni mahali pakulala na siyo mahali pakupiga kelele, mazungumzo ya bwenini yawe ya maana na siyo matusi au lugha mbaya.
2. Mwanafunzi akitoroka bwenini usiku kwenda popote atakuwa amejifukuzisha shule.
3. Muda wa darasani hairuhusiwi kuwepo bwenini, atakayebainika kuwepo bwenini wakati wa vipindi atafukuzwa shule.
4. Ni marufuku kuwasha moto bwenini, Kuwasha vyombo vya umeme kama vile:- pasi, hita, au kufanya ufundi wa aina yoyote ile kwenye miundombinu ya umeme Usafi wa bweni ni wajibu kwa kila mwanafunzi anayeishi bweni husika.
5. Ni marufuku mwanafunzi kuingiza au kula chakula cha aina yoyote bwenini.
6. Ni marufuku mwanafunzi kuingiza mgeni yeyote ndani ya bweni.

**D. SHERIA ZA UKUMBI WA CHAKULA.**

1. Kila mwanafunzi aliye chakula chake ndani ya ukumbi wa chakula, na afuate utaratibu uliowekwa wa matumizi ya ukumbi wa chakula mf. Mpango wa usafi wa ukumbi wa chakula na mpango wa kukaa ndani ya ukumbi wa chakula
2. Wakati wa chakula kelele hazitakiwi.
3. Kila mwanafunzi anatakiwa awe na tabia nzuri mezani, umwagaji hovyo wa chakula hauruhusiwi.
4. Usafi lazima ufanywe mara baada ya chakula.
5. Mwanafunzi hatakiwi kuingia jikoni bila ruhusa, ni marufuku kwa mwanafunzi kupika chakula chake binafsi jikoni.

6:0. **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE.**

1. Wizi.
2. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
3. Uvutaji wa bangi.
4. Makosa ya jinai
5. Unyanyasaji wa kijinsia au kimadarasa.
6. Kupigana au kumpiga mwalimu.
7. Kudharau Bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa
8. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
9. Kuoa /kuolewa au kujihusisha na mapenzi.
10. Kupata mimba au kusababisha kupata mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoa mimba
12. Kutofanya mazoezi na mitihani ya shule bila sababu ya msingi.
13. Kutohudhuria shule kwa muda wa siku 90 mfululizo bila sababu ya msingi.
14. Kugoma, kuchochea au kutishia usalama wa watu au mali ya umma.
15. Kukataa adhabu halali kwa makusudi.
16. Kutumia SIMU shuleni. **(Usije na simu shuleni).**
17. Kushiriki matendo ya uhalifu.
18. Kutembelea majumba ya starehe, nyumba za kulala wageni na nyumba za watumishi wa shule.
19. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
20. Udanganyifu wa mitihani ya ndani na nje ya shule

**UTARATIBU WA ADHABU.**

1. Mwanafunzi yeyote anayepewa adhabu lazima aifanye, ujeuri au ubishi wa aina yoyote utasababisha kuongezwa kwa adhabu hiyo. Kosa la kugomea adhabu linahesbiwa kuwa ni utovu wa nidhamu usiovumilika.
2. Mwalimu/walimu watamwadhibu mwanafunzi yeyote anayekiuka sheria/taratibu/kanuni za shule au bweni zilizowekwa.
3. Mwanafunzi atapewa adhabu kulingana na kosa alilolifanya.
4. Mkuu wa shule anaweza kutoa adhabu kwa makosa makubwa kwa kumwadhibu mkosaji/kumsimamisha masomo kwa muda au kwa kupitia Bodi ya shule mwanafunzi anafukuzwa shule.

**Ninakutakia maandalizi mema,**

**KARIBU SANA SHULENI.**

..........................

**HAJI S. SALUM**
**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
URAMBO SEKONDARI
S.L.P. 211
URAMBO.

**KIAMBATANISHO 'C'**

**A. FOMU YA KUKUBALI KUANDIKISHWA SHULENI**

(Ijazwe na kukabidhiwa kwa msajili wa wanafunzi siku ya kuripoti shuleni kwa mara ya kwanza)

1. Jina kamili la mwanafunzi, kama lilivyo katika SELFORM (kwa herufi kubwa zote).
   ……………………………………………………………………
   Tarehe e ya kuzaliwa ……………………………………………………………
3. Mahali alipozaliwa (Wilaya) ………………………………………………
4. Uraia ……………………………………………………………………
5. Shule anayotoka ………………………………………………………...
6. Dini ……………………………………………………………………..
7. Dhehebu …………………………………………………………………..
8. Nyumbani ni: Mkoa ……………………………… Wilaya ………………
9. Jina kamili la mzazi/mlezi ……………………………………………
   Uhusiano na mlezi kama hana mzazi ……………………………………...
   Anuani ya mzazi/mlezi ……………………………………………………
   Namba ya simu ya mzazi/mlezi …………………………………………
   (Mabadiliko yawasilishwe Ofisini mara moja) ……………………………

**10. Ahadi ya mwanafunzi.**

(a) Mimi ………………………………………………… Nakubali nafasi ya shule hii niliyopewa. Naahidi kutii KIKAMILIFU sheria na kanuni zote za shule wakati wote niwapo mwanafunzi wa shule ya sekondari Urambo, naahidi kwamba sitashiriki katika migomo, fujo na makosa mengine ya jinai, na kwamba UTORO KWANGU UTAKUWA NI MWIKO.

(b) Ninaahidi kwamba kamwe sintachelewa kurudi shule mara likizo inapokwisha na kwamba nikichelewa nitakubali adhabu zote zitakazotolewa ikiwemo kurudishwa nyumbani n.k.

(c) Nitasoma kwa bidii ili kufikia wastani wa shule ambao mwisho ni Division III nakwamba nisipofanya vizuri katika mitihani ya ndani nitabaki shule wakati wa likizo kwa ajili ya masomo ya ziada kwa gharama za mzazi/mlezi.

(d) Kamwe sintalala Bwenini wakati wa vipindi kwani kosa hilo linaweza kunifukuzisha shule.

(e) Ndugu wafuatao ndio watakaoruhusiwa kuja kuniona au kutoa msaada ninapopata tatizo.

| SN | JINA KAMILI | UHUSIANO | NAMBA YA SIMU | PICHA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |

Saini ya mwanafunzi ........................................ tarehe .......................

11. Ahadi ya mzazi/mlezi.

(a) Nakubali mwanangu ........................................................ Ajiunge na shule ya sekondari Urambo katika kidato cha ..................... Mwaka ............
Na ninaahidi kwamba NITAKUWA NALIPA KARO PAMOJA NA MICHANGO MINGINE YOTE YA SHULE KWA WAKATI ULIOWEKWA HADI HAPO ATAKAPOHITIMU KIDATO CHA SITA.

(b) Nitahakikisha mwanangu anarudi shule baada ya likizo katika tarehe iliyopangwa na shule na si vinginevyo, na ikitokea sababu ya msingi kwa mwanagu kuchelewa shule nitatoa taarifa siku tatu kabla ya tarehe ya kufungua shule na kuambatanisha na uthibitisho wa daktari iwapo sababu hiyo ni ugonjwa.

Jina kamili la mzazi/mlezi ..................................................................
Anuani ya mzazi/mlezi ....................................................................
Saini ya mzazi/ mlezi ........................................tarehe .......................

**ILANI**

**(i) Mwanafunzi hatasajiliwa kama fomu hii haitajazwa kikamilifu.**

**KIAMBATANISHO 'D'**
**(To completed by a Government Medical Officer and returned to the Headmaster)**
**GOVRNMENT OF TANZANIA**
**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**TO THE MEDICAL OFFICER**
**…………………………………** **FROM ……………………**
**…………………………………** **DATE: ……………………**
**MR/MRS/MISS**

___________________________________________________________

**(Name in full)**

Please examine the above named as to his/her physical and fitness for full time of his/her Training
Course. (Form five to six). The examination should include the following categories.

I a) Eye
 b) Hearing
 c) Limbs
 d) Speech
 e) Venereal Diseases
 f) TB
 g) Leprosy
 h) Epilepsy

II Neuroses

III Pregnancy

IV Other Serious Disease

**(To be completed a Government Medical Officer)**
I have examined the above named and consider that/she/he is physical and mentally fit/unfit for a full time student training course.

I. a) Eye sight ……………………………………………………..
 b) Hearing ……………………………………………………
 c) Limbs ……………………………………………………..
 d) Speech ……………………………………………………
 e) Venereal Diseases ………………………………………
 f) TB …………………………………………………………
 g) Leprosy ……………………………………………………
 h) Epilepsy ……………………………………………………

II NEUROSES ……… ……………………………………..

III Pregnancy ……………………………………………………

IV Other serious Diseases ………………………………………..

**DATE : ………………………….. SIGNATURE: ……………………..**

**STATION: ……………………… DESIGNATION: ……………………**